# Mfululizo wa mafunzo ya usafi wa mazingira na usafi binafsi katika miji midogo, Babati-Tanzania

## Februari 2021

▼ Moja kati ya masoko ya wazi katika mji wa Babati, Tanzania.




## Ujumbe muhimu

1. Utambuzi wa washirika husika (serikali, watoa huduma, asasi za kiraia, wakufunzi, nk) ni muhimu katika mchakato wa mipango.
2. Ushirikishwaji wa wizara husika na wadau katika kila hatua ya mchakato wa utafiti ni suala muhimu katika kuhakikisha umiliki wa mradi na matokeo ya tafiti.
3. Ushirikishwaji wa serikali za mitaa katika ukusanyaji wa taarifa ni muhimu na uliongeza uwezekano wa kufikia maeneo mengi ya miji na ushiriki wao katika tafiti ulirahisisha mchakato wa kukubali matokeo ya tafiti na hivyo tafiti hii kuingizwa katika mipangokazi ya maendeleo.
4. Uandazi wa mfumo mkuu ufanyike kwa kujali dhana ya ushirikishwaji baada ya mchakato wa mipango. Hii itaruhusu ushirikiano mzuri katika utatuzi utakaovumbuliwa na mapendekezo katika namna ya ushirikishwaji kwa ajili ya maslahi ya mpango wa maendeleo kwenye mji.

WaterAid

# 1. Utangulizi na muktadha

Lengo la ripoti hii fupi ni kutoa matokeo makuu ya utafiti uliofanywa na shirika la WaterAid Tanzania katika mji mdogo wa Babati na kuainisha vipengele muhimu vya kuzingatia katika matazamio ya ukuaji wa miradi.

Nchini Tanzania, ongezeko la makazi yasiyo katika mpangilio imepelekea kuongeza changamoto ya upatikanaji wa huduma za usafi wa mazingira na usafi binafsi katika sehemu za mjini. Inakadiriwa kuwa ni 34.2% tu ya idadi ya watu waishio mjini wanapata huduma za vyoo bora huku waliobakia wakitumia vyoo vya kawaida au kujisaidia katika mazingira ya wazi (NBS,2014). Katika upande wa vifaa vya kunawia mikono, chini ya 25% ya idadi ya watu (mjini na vijijini) wana sehemu maalum za kunawia mikono kwa maji safi na sabuni (URT, 2014). Zaidi, ni 38% tu ya shule zenye idadi ya vyoo toshelezi kulingana na mahitaji; 20% ya shule zina maji ndani ya eneo la shule na chini ya 10% ya shule nchini ina vifaa hai vya kunawia mikono vyenye maji vyenye kuwezesha watoto kudumisha usafi binafsi na kuwa na tabia endelevu ya kutunza mazingira ikiwemo vyoo (URT,2014).

Ingawa Tanzania imeahidi kuongeza upatikanaji wa vyoo bora kufikia 95% ya idadi ya watu hadi mwaka 2025, magonjwa ambukizi yanayohusiana na upatikanaji wa maji, usafi wa mazingira na usafi binafsi yanabakia kuwa tishio kubwa na kupelekea matumizi ya zaidi ya bilioni 301 za kitanzania kila mwaka (WSP,2012). Maeneo yanayoathirika zaidi ni miji midogo ambayo inakua kwa kasi bila kuwa na mipango miji elekezi pamoja na upatikanaji wa mahitaji muhimu kama vile maji, vyoo bora, vifaa vya kunawia mikono pamoja na huduma za kijamii kulingana na idadi ya watu inavyokua kwa kasi.

Kwa ukuaji na maendeleo katika maeneo yanayokua kwa kasi, shirika la WaterAid Tanzania kama moja washiriki wa utafiti wa Sanitation and Hygiene Applied Research for Equity (SHARE), walifanya utafiti shirikishi katika mji wa Babati kwenye vipengele vya usafi wa mazingira na usafi binafsi wakishirikiana na taasisi ya Nelson Mandela African Institution of Science and Technology (NM-AIST), halmashauri ya mji wa Babati, Mamlaka ya maji ya Babati, (BAWASA), na Sekretariati ya mkoa wa Manyara katika kipindi cha mwaka 2016-2018.

Kuelewa muktadha wa Babati, kutamsaidia msomaji wa ripoti hii kuelewa mbinu na mafunzo katika mwelekeo chanya, Hata hivyo, tunategemea utafiti wa kesi wa Babati utaongeza mwanga kwenye njia na vigezo ambavyo taasisi zinazofanya maamuzi ya maendeleo kuweka kipaumbele katika masuala ya usafi wa mazingira na kuwekeza katika kubadili tabia ya usafi binafsi katika miji inayokua kwa kasi.



WaterAid

# 2. Mwanzo wa mradi, mpangokazi na mbinu bunifu

## Mwanzo wa mradi

Vigezo kadhaa vilitumika kubainisha mji utakaofaa kutumika katika utafiti huu. Kikubwa kabisa, mji huo ilikua lazima uwe sehemu ambayo WaterAid wanafanya kazi au kuwa katika mpangokazi wa shirika katika siku za mbeleni. Kwa kutumia kigezo hiki kama kianzio, miji miwili ilichaguliwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu mnamo mwezi Julai mwaka 2015 ambayo ni halmashauri ya Babati pamoja na Halmashauri ya Geita. Ili kuchagua mji utakaolandana na mahitaji ya tafiti, vigezo vifuatavyo vilizingatiwa:

- Uongozi na rasilimali watu,
- Utayari wa serikali za mitaa,
- Uwazi na utayari wa ushirika,
- Uwepo wa mipangokazi na huduma,
- Rasilimali fedha.

Kulingana na vigezo tajwa hapo juu, mji wa Babati ulichaguliwa kufanyiwa utafiti. Mji wa Babati una idadi ya watu 110,000 wenye kilomita za mraba 460.86 na uko katikati ya mkoa wa Arusha, Dodoma, Singida, Mbulu na Simanjiro. Mkoa wa Manyara ambao kunapatikana wilaya ya Babati uliundwa mwaka 2002 na mji wa Babati uliidhinishwa kama makao makuu ya mkoa mwaka 2004. Shughuli kuu ya maendeleo katika mji wa Babati ni kilimo ambacho ni kivutio kwa wawekezaji katika eneo hilo.

Hadi kufikia mwaka 2019, mji wa Babati haukua na miundombinu bora ya majitaka au sehemu za kuhifadhia takangumu. Kuna kreta mbili nje ya katikati ya mji wa Babati maalum kwa ajili ya kutupia aidha taka ngumu au taka maji. Sehemu hizi haziko katika mpangilio au katika usalama kwa makazi na afya za wananchi.

## Mbinu na mpangokazi

Mbinu ya mpango shirikishi kwa ajili ya usafi wa mazingira katika mji wa Babati ulifuata hatua zifuatazo kama zilivyoelezewa kwa kifupi hapa chini:

- **Ushirika:** Mradi uliendeshwa kwa kushirikia na chuo cha Nelson Mandela African Institution of Science and Technology (NM-AIST), halmashauri ya mji wa Babati, Mamlaka ya maji ya Babati, (BAWASA), na Sekretariati ya mkoa wa Manyara. Majukumu, kazi na umuhimu wa wadau walioshirikisjhwa ulifanyiwa tathmini kwa kutumia mfumo wa ushirikishwaji wa shirika la WaterAid (Beale et al., 2018)
- **Uanzilishi:** kulifanyika warsha ya kuzindua utafiti kabla ya kuanza kukusanya taafira ili kujenga uelewa sawia baina ya wadau kuhusiana na lengo la utafiti, muda wa mradi, matarajio na mgawanyo wa majukumu.
- **Ukusanyaji taarifa na utafiti:** Utafiti wa nyumba kwa nyumba katika kaya 20,000 ulifanyika na kukusanya taarifa kuhusiana na hali ya usafi wa mazingira ya mji sambamba na matumizi ya njia za ubora na kiasi ambazo ziliangalia hali ya kijamii, utamaduni, uchumi katika mji na hali ya usafi wa mazingira pamoja na usafi binafsi kabla na wakati wa ukusanyaji data. Lengo lilikuwa ni kuelewa namna kaya na taasisi zinahamasishwa na kuwekeza katika usafi wa mazingira pamoja na binafsi na vihatarishi vinavyopelekea mabadiliko ya tabia. Moja ya tokeo kubwa katika utafiti huu ilikua ni uundwaji wa Shit Flow Diagram inayoonyesha uwiano wa taka kama zinaweka kutunzwa kwa usalama au la.
- **Uchunguzi wa kiuchumi:** Uchunguzi wa kiuchumi ulifanyika ili kupata uelewa wa vitu vinavyosukuma taasisi za binafsi au serikali kuwekeza katika kuboresha huduma zinazohusiana na usafi wa mazingira na usafi binafsi katika maeneo ya mjini. Utafiti huu ulifanyika katika mji wa Babati, Bomang'ombe, Halmashauri ya mji wa Moshi, jiji la Arusha na manispaa ya Temeke jijini Dar Es Salaam.
- **Ushirikishwaji wa jamii:** Utaratibu huu ulieleweka kama mfumo wa kushirikisha jamii katika mradi na kupata maoni yao kupitia mfumo huu. Matokeo ya tafiti yalitangazwa na kujadiliwa katika ngazi ya kata katika warsha tofauti tofauti.
- **Uingizwaji wa tafiti katika mpangokazi mkuu uliopo:** Mara kwa mara, mshauri alikua akifanyia kazi mpangokazi mkuu wakati utafiti wa mradi huu ukiendelea hivyo ikawa rahisi kuainisha tafiti hii katika mpangokazi huo ambao ulikua ukifanya kazi tayari kwa kuongeza baadhi ya vipengele ambavyo vilionekana kuwa na umuhimu kwenye suala la usafi wa mazingira.
- **Mipango ya matukio:** Mtiririko wa matukio ulifanyika kulingana na utafiti katika warsha iliyofanyika mjini Babati. Lengo la warsha hii lilikua ni kupima uelewa wa wadau shirika kuhusu hali ya usafi mazingra na binafsi katika mji wa Babati, kupata suluhisho kuhusiana na masuala ya usafi wa mazingira na usafi binafsi na kutengeneza mpango kazi.
- **Uundwaji wa mpango wa biashara:** Mojawapo ya mipango ya kusaidia mji wa Babati katika masuala ya usafi wa mazingira na usafi binafsi, kulitengenezwa mpango mfano wa biashara kulingana na matukio yalichaguliwa katika tafiti.

# 3. Matokeo

## Viashiria vya idadi ya watu

Mji wa Babati una idadi ya watu 110,000.

85% ya kaya zinamiliki nyumba zao binafsi huku 11.5% ya kaya zikiwa katika makazi ya kupangisha. Zaidi, uwiano wa idadi katika kaya moja ni watu watano na 50.4% ya kaya zina watoto chini ya miaka mitano huku 49.6% ya kaya zikiwa hazina watoto chini ya miaka mitano.

Zaidi ya nusu ya waliohojiwa walikua wakijishughulisha na kilimo kama njia kuu ya kujiingizia kipato na 60% ya watu wakiwa na elimu ya msingi. Wafanyakazi wanaopokea mshahara walikadiriwa kuwa 8% na uwiano wa kipato kwa mwezi ilikua dola za kimarekani 96.

## Hali ya usafi wa mazingira na usafi binafsi katika mji wa babati


Menejimenti ya majitaka katika mji wa Babati unategemea zaidi miundombinu maeneo maalumu yaliyotengwa kwa ajili yake. Kulingana na utafiti, 90% ya kaya zinamiliki vyoo huku 7.4% ya kaya zikitumia vyoo kwa pamoja. Vyoo vya shimo ndio ambavyo vipo katika kaya nyingi huku 42% ya vyoo hivyo vikiwa vimesakafiwa.

Nusu ya kaya hutoa taka katika vyoo vyao pindi vinapojaa na kisha kuendelea kuvitumia huku nusu ya kaya zilizobaki huvitelekeza na kuchimba vipya. Hakuna mtambo wa kutibu takamaji au takangumu.

Mifumo ya utupaji taka katika mji wa Babati kwa 7% ni kuzifukia katika shimo karibu na nyumba, wakati 49% ya kaya zikitupa taka kwa kuzipeleka katika eneo moja la wazi lililo kilomita tano nje ya mjii wa Babati. Uchunguzi kupitia mfumo wa SFD unaonyesha kuwa 69% ya taka katika mji wa Babati hazitunzwi/ kutupwa vyema hivyo kuwaweka wananchi wa mji huo katika hali hatarishi kiafya. (mchoro namba 1).



WaterAid




**Mchoro 1** - Mfumo pendekezwa wa majitaka Babati.

Kwa upande wa usafi binafsi, wengi wa wananchi wanatambua umuhimu wa usafi binafsi japokua ni 21% tu ya kaya ndio wenye sehemu maalum za kunawia mikono.

Njia iliyozoeleka ya kutibu maji ya kunywa ni kwa kuyachemsha (82%) ikifuatiwa na kuweka klorini katika maji, ingawa ni 45% ya wananchi ndio walijibu kuwa wanatibu maji yao. Baadhi ya matukio ya uchafu wakati wa hedhi pia yaliripotiwa.

## Sera na mipangilio ya taasisi

Mashirika ya kiserikali kama vile halmashauri ya mji wa Babati yana mamlaka ya kuweka sheria na kusimamia utekelezaji wake. Kuna idara kadhaa katika halmashauri ya mji wa Babati zinazoshughulika na usafi wa mazingira ila hazina muunganiko wa mawasiliano baina yao. Mara kadhaa kumekua na marudio ya nguvukazi na upungufu wa kumbukumbu katika taasisi. Wakati wa tafiti kipengele cha uchunguzi wa uchumi katika mji wa Babati, iligundulika kuwa ukosekanaji wa fedha, mipango duni, kutokua na nia pamoja na kukosekana na mfumo elekezi ni baadhi ya vitu vichache vinavyosababisha kukosekana kwa uwekezaji katika masuala ya usafi wa mazingira katika mji wa Babati.

## Upatikanaji wa fedha: Chanzo na maamuzi makuu kwa ajili ya uwekezaji

Kwa ujumla nchi nzima, mara nyingi wanasiasa na viongozi hawaoni thamani katika kuwekeza kwenye usafi wa mazingira kwasababu suala hili halina mchango mkubwa katika maslahi ya kisiasa. Hii inamaanisha kuwa uwekezaji kwenye usafi wa mazingira katika ngazi za tawala za mikoa na serikali za mitaa unaweza kutokea endapo tu kama viongozi wataguswa kipekee ili wajisikie sawia na msukumo wa jamii ili waweze kuwekeza katika usafi wa mazingira kama wanavyofanya kwenye menejimenti ya maji taka.

Halmashauri ya mji wa Babati inapokea maagizo na miongozo kutoka serikali kuu kuhusiana na bajeti pamoja na matumizi. Mgawanyo wa fedha unafanyiwa maamuzi na kamati za maendeleo ngazi ya kata ijapokua na uelewa/mgawanyo mdogo wa fedha kwenye sekta ya usafi wa mazingira. Suala la usafi wa mazingira halipewi kipaumbele. Hivyo basi, Halmashauri ya mji wa Babati inabidi kutumia bajeti yake ya ndani kwa ajili ya kuwekeza katika usafi wa mazingira. Kabla ya mradi huu, takribani 3% ya bajeti ya halmashauri ya mji ilitumika katika usafi wa mazingira, usafi binafsi na maji kwa kipindi cha mwaka mzima.

Katika utafiti huu iligundulika kuwa ushawishi wa kutenga bajeti katika ngazi ya kaya kwa ajili ya usafi wa mazingira na usafi binafsi unategemea na kiwango cha elimu, na pia kiwango cha kipato pamoja na uwepo wa huduma shirikishi kama vile upatikanaji/ uwepo wa maji. Hata hivyo, ushawishi mkubwa wa kutumia au kujenga vyoo vya aina yoyote ni kutokana na kuogopa sheria zilizopo, kuogopa mlipuko wa magonjwa, kutaka kuonekana na hali nzuri ya kiuchumi katika jamii na kuhitaji kuwa na sehemu salama ya kujisaidia.

Kwa taasisi kama vile serikali za mitaa, mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika binafsi, nk utawala bora ni kiungo muhimu katika kuwezesha ushiriki na uwekezaji katika masuala ya usafi wa mazingira na usafi binafsi.

Utawala bora unahakikisha ufanisi wa taasisi, kujenga uwezo, mwelekeo wa wazi ya malengo ya sera, na ugawaji wa rasilimali za kifedha, ushirikishwaji wa asasi za kiraia na uwepo wa uwezeshwaji wa sharia (sheria mama na sheria ndogo ndogo).

## Mtiririko wa mapendekezo ya usafi wa mazingira na usafi binafsi

Mtiririko wa mapendekezo yalitanguliwa na uchukuaji wa maono/ malengo ya mji wa Babati. Machaguo kadhaa kuhusiana na usafi wa mazingira na usafi binafsi yalitolewa kutoka kwa watendaji wakuu (watendaji wa serikali kuu, watendaji wa serikali za mitaa, wawakilishi wa jamii, watafiti, timu ya shirika la WaterAid pamoja na wadau wengine wa usafi wa mazingira na usafi binafsi). Ni muhimu kufahamu kwamba uchaguaji wa mtiririko huu wa mapendekezo ulifanyika na washiriki tajwa wote hapo juu baada ya kufanyika kwa uchunguzi wa mapungufu, fursa, ogofyo na uwezo wa halmashauri ya mji wa Babati katika upande wa usafi wa mazingira na usafi binafsi. Kisha, mawasilisho ya faida na hasara za kila pendekezo na pia masharti ya utekelezaji wa kila pendekezo.



WaterAid

Mapendekezo matatu kwa ajili ya usafi wa mazingira ni kama yafuatavyo:

1. Usimamizi wa Majitaka – kuwepo kwa mfumo utakaoweza kutunza, kuchukua, kutibu, kutumia tena na kumwaga taka zitakazokua katika sehemu ambapo taka za kinyesi zinapelekwa.
2. Majitaka – Uwepo wa mtandao wa mabomba makubwa utakao safirisha majitaka katika mtambo tiba wa taka hizo.
3. Mbadala wa mfumo wa majitaka – Mfumo wa usimamiza majitaka Babati.

Pendekezo lililochaguliwa lilikua usimamizi wa majitaka, ambapo kuna faida nyingi:

- Unafuu katika uendeshaji na usimamizi
- Rahisi kusimamia
- Matumizi kidogo ya nishati
- Matumizi kidogo ya fedha kwa upande wa mjini
- Haihitaji mtaji mkubwa kama mifumo mingine
- Inatoa fursa kwa wakulima na watumia nishati kutumia taka zinazozalishwa baada ya kutibiwa katika mtambo
- Inatoa nafasi ya uvumbuzi wa kitaalamu.

Mtiririko wa mapendekezo upande wa usafi binafsi:

1. Mbinu ya mwingiliano- Kutekelezwa kupitia programu za WASH katika ngazi ya kaya.
2. Mbinu ya ujumuishi- Kuweka pamoja afya, elimu, lishe, kilimo na sekta binafsi kupitia taasisi.
3. Mbinu ya kampeni- Kutekelezwa nchi nzima, au katika wilaya/mji katika kipindi cha muda mfupi mfupi kwa kutumia mitindo iliyoundwa kwa ajili ya kampeni hiyo.

Ilikubalika kwa wadau kuunganisha mbinu ya mwingiliano pamoja ujumuishi kwa pamoja.

Mipango iliyochaguliwa ilisemekana kuwa itaendana vyema na mpango mkuu wa mji wa Babati.



WaterAid

# 4. Sababu za mafanikio

## Ushirikishwaji wa serikali wakati wa kukusanya taarifa

Ushirikishwaji wa serikali katika ukusanyaji wa taarifa hizi uliongeza matokeo ya fursa ya kufikia maeneo mengi zaidi katika mji na ushiriki wao katika tafiti hii ulihakikisha utayari wao wa kukubali matokeo na kusaidia utafiti kujumuishwa katika mipango ya maendeleo.

## Ushirikiano

Utambuzi wa wadau husika ni muhimu katika kuandaa mipano ya maendeleo. Shirika la WaterAid kwa kushirikiana na NM-AIST, BTC,BAWASA na Sekretariati ya mkoa wa Manyara waliongoza mchakato mzima wa mipango na kila mdau alifanya jukumu lenye manufaa:

- NM-AIST alikua kiongozi msaidizi wa viambata vyote vya tafiti. Walihakikisha taarifa zinakusanywa na upembuzi wa tafiti unafanyika kwa makini ili kupelekea mtiririko wa mipango.
- BAWASA walitoa watu wenye ujuzi wa kiufundi, wataalamu wa maji na usafi wa mazingira.
- BTC ilifanikisha wadau wengine kufanya kazi yao kwa urahisi kwa kuwapa taarifa na maarifa yanayohitajika na kwa kuwaunganisha kwa wadau watakaohitajika kwa ajili ya kurahisisha zoezi la utafiti. Waliweza pia kuwasiliana na wananchi/jamii kuhusiana na utafiti.
- Sekretariati ya mkoa wa Manyara iliratibu na kusimamia utekelezaji wa utafiti na kuchochea ushiriki wa halmashauri ya mji wa Babati na BAWASA katika mchakato wa utafiti.

## Uhamasishaji wa wadau

Uwepo wa wadau husika katika utafiti ilikua ni moja ya fanikio kubwa, Hakika, mradi ulitambulishwa kwa wadau wote muhimu na timu ya mradi uliweka maazimio ya kuona mabadiliko ya tabia katika kipindi cha uhai wa mradi. Ili kufikia malengo hayo, wadau walishirikishwa katika kila hatua kupitia mafunzo ya kutembelea katika miji mingine na kualikwa katika vikao muhimu vya mradi. Moja ya matokeo ilikua ni baina ya wakurugenzi BTC na BAWASA ambao waliweza kuona mafanikio ya mbinu za usafi wa mazingira na kusaidia kubadili mtazamo wao kuhusiana na usimamizi wa majitaka.

## Kujenga uwezo

Ilikua ni muhimu sana kujenga uwezo kwa watenda kazi haswa wakufunzi kutoka chuo kikuu ili kuhakikisha ubora wa taarifa zitakazokusanywa na upembuzi wake. Mradi huu wa utafiti ulisaidia kujenga uwezo kwa wadau katika maeneo yafutayo:

- Ushirikiano na chuo kikuu cha Leeds ulisaidia timu ya utafiti kutengeneza mfumo wa majitaka Babati ya mji wa Babati.
- Wanafunzi wawili wa uzamili katika chuo cha NM-AIST walimaliza utafiti wao kuhusiana na Babati na kuuchapisha.
- Ushiriki wa BTC na BAWASA ulisaidia timu ya utafiti kujenga utafiti na kuandaa ujuzi. Kutokana na motisha ya awali ya kifedha katika mradi uliotengenezwa na BAWASA katika mwaka wa kwanza, hadi kufikia motisha ya kina inayohusiana na kujenga uwezo kwa watumishi wake.
- Kupitia msaada kutoka SHARE, mafunzo kuhusiana na ukusanyaji data zenye ubora yalitolewa kwa timu ya utafiti.
- Msaada wa kiufundi mara kwa mara ulipokelewa kutoka kwa mkurugenzi wa tafiti kutoka SHARE.

## Mawasiliano na kuongeza uelewa

Ushirikishwaji wa wizara husika na wadau katika kila hatua ya mchakato wa utafiti ni suala muhimu katika kuhakikisha umiliki wa mradi na matokeo ya tafiti. Halmashauri yam ji wa Babati na BAWASA sasa ndio viongozi wanaohakikisha mapendekezo yaliyotokana na utafiti huu kuhusiana na usafi wa mazingira na usafi binafsi yanatekelezwa. BAWASA wamejumuisha matokeo ya utafiti huu katika mpango wao wa kibiashara na wanafanya kazi bega kwa bega na shirika la WaterAid paamoja na wadau wengine katika utekelezaji wa FSM wakiwa na lengo la kutafuta fedha kwa ajili ya kuwezesha mpango huo.

# 5. Fursa za muendelezo

Yafuatayo yalikua mambo muhimu kuhusiana na BTC yaliyosaidia kufanya mradi kufanikiwa kwa kiwango cha juu:

- Uwazi wa mamlaka ya serikali za mitaa kuhusiana na ufikishaji wa huduma za usafi wa mazingira,
- Kujitolea na kujituma kwa serikali na sekretariati ya mkoa wa Manyara katika kuhuisha huduma za usafi wa mazingira katika mji wa Babati,
- Uwepo wa bingwa wa masuala ya WASH katika ngazi ya BTC,
- Fursa za kujengewa uwezo,
- Mwendelezo wa mchakato wa mipango ya maendeleo,
- Mfadhili kuvutiwa na mji,
- Uhusiano kati ya watafiti na wafanya maamuzi.

# 6. Ukuaji wa mradi

Masuluhisho lazima yaendane na uhalisia kulingana na taarifa zilizokusanywa ingawa inatambulika kwamba utafiti uliofanyika katika mradi huu ulikua wa gharama sana kuigwa tena katika miji mingine. Uwezeshaji wa kifedha unaweza kuwa kizuizi na hivyo kufanya utafutaji wa fursa za uwezeshaji mdogo wa kifedha unaweza ukawa namna inayofaa kwasababu hela ya mfadhili inaweza isiwe inapatikana kila mara itakapoombwa kwa ajili ya kufanya kazi za kitafiti.

Hivyo basi, ni muhimu kupunguza mchakato wa taarifa zitakazokusanywa kwa kutegemea zaidi taarifa zisizo mama na kuzipa kipaumbele wakati wa kukusanya taarifa pale zitakapohitajika. Kwa kuongezea, uandaaji wowote wa mpango mkakati mkuu ufanyike kulingana na mtiririko wa mchakato wa mipango. Hii itasaidia ushirikiano mzuri katika mpango mzima wa mji ambao utahamasisha ugawaji wa majukumu kwa watenda kazi katika mji. Katika mfano wa Babati, mchakato ulibadilishwa, wakandarasi waliohusika katika mchakato wa mipango walikua na mapendekezo ya mfumo wa majitaka unaounganisha mji mzima wa Babati. Baada ya kuunganisha miradi hiyo miwili, watendaji kazi waligundua kuwa hili ni jamba ambalo halina mantiki/haliwezekani kutokana na ufinyu wa rasilimali kati ya halmashauri ya wilaya ya Babati na Mamlaka ya maji ya Babati.

# 7. Hitimisho

Ukuaji wa miji, huja na fursa nyingi ila huleta changamoto nyingi vilevile. Utafiti huu umesaidia kuainisha umuhimu wa kuingiza mifumo ya WASH katika mipango miji. Ila pia umeainisha kuwa mipango bora na ushirika wa wadau unasaidia kuhakikisha miji midogo ina mifumo endelevu ya usafi wa mazingira na usafi binafsi.

Kuwashirikisha watenda kazi, wakiwemo wanajamii, kwa maana ya matukio ya usafi wa mazingira na usafi binafsi kulingana na mazingira ya eneo husika na suluhisho zilizopendekezwa. Ingawa, utekelezaji bora wa suluhishi hizi, kupitia utafutaji wa rasilimali za uchumi, iwe ngazi ya taifa au kimataifa ni kielelezo bora kabisa cha mafanikio ya mbinu zilizoundwa. Hivyo basi, elimu inabidi iwe endelevu kwa ajili ya ukusanyaji wa wafadhili na watenda kazi katika masuala ya upatikanaji wa fedha na utekelezaji.

## Shukrani

Waraka huu umeandikwa na Mbaye Mbéguéré (Uniti ya usaidizi wa program, WaterAid UK) pamoja na Joanne Beale (Mshauri) na majumuisho ya ushauri yakinifu kutoka kwa Kyla Smith na Om Prasad (PSU). Shukrani za kipekee za Remi Kaupp (PSU) kwa mchango wake kwa Joseph Banzi na Abel Dugange (WaterAid Tanzania) na kwa timu ya NM-AIST.

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| BTC | Halmashauri ya mji wa Babati |
| BAWASA | Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira, Babati |
| FSM | Usimamizi wa Majitaka |
| LGA | Mamlaka ya serikali za mitaa |
| NM-AIST | Chuo  Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela |
| PEA | Uchambuzi wa Siasa ya Uchumi |
| SFD | Mchoro wa Mtiririko wa Kinyesi/uchafu |
| SHARE | Taasisi ya Usafi wa mazingira, Usafi binafsi kwa ajili ya usawa |
| SWOT | Uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa na Vitisho |

## Marejeleo


- Beale et al. (2018). *Building partnership for participatory sanitation and hygiene planning: lessons and experiences from Tanzania.* WEDC Conference Paper.
- NBS (2014). Basic demographic and socio-economic profile. Dar es Salaam, Tanzania.
- Pilgrim et al. (2007). *Principles of Town Water Supply and Sanitation. Part 1: Water Supply.* The World Bank. Washington DC.
- URT (2014) National Sanitation Campaign Implementation Guideline. Ministry of Health and Social Welfare
- Water and Sanitation Program (WSP) (2012), *Economic impacts of poor sanitation in Africa.*

# Kwa mawasiliano zaidi

Unaweza ukapata maelezo zaidi kwa kubofya kiungo hiki
**https://washmatters.wateraid.org/small-town-sanitation**

Hii ni sehemu ya mtiririko wa maelekezo ya kujifunza kuhusu usafi wa mazingira katika miji midogo.



WaterAid/ Joseph Banzi

▲ **Uwasilishaji wa mchoro unaoonyesha mteremko wa uchafu/ kinyesi kwa mamlaka ya mji wa Babati, Tanzania, Julai 2020.**



WaterAid